

Nafasi

Acha sentimita 45 katikati ya mistari na 20 katikati ya mimea.

Mbolea

Tia nusu ngunia ya mbolea ya DAP kwa eka (kilo 25 kwa eka) na ichanganywe vyema na udongo kabla ya kufunika mbegu.

Upaliliaji

Palilia mara ya kwanza wiki mbili baada ya kuchipuka na mara ya pili kabla ya kuota maua.

Ulinzi wa mmea

Wadudu ni kama vile:

- Wadudu wa kuruka wakati wa kupanda
- Wadudu weusi - hutokea sana wakati wenye baridi bila mvua
- Wadudu wa majani - wakati wa kuota majani
- Wadudu wa kutoboa wakati mbegu inapokua
- Wadudu waharibifu wakati wa kuhifadhi.

Kuzuia maradhi na wadudu

Kemikali za kuzuia wadudu hawa hupatikana katika maduka yanayonza bidhaa za kilimo (Agrovet).



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Watayarishaji:

Karanja, D.R., Mulwa, D, M'Ragwa, L na Rubyogo, J

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkuu wa Kituo,

KARI Katumani

S.L.P. 340, 90100


Machakos

Simu/Nukulishi: 020 2311449

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 13 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Kuza marahagwe yaliyoimarishwa kwa chakula na mapato



Utangulizi

Maharagwe ni mmea muhimu sana wa chakula katika sehemu za urefu wastani, na zisizo kame sana nchini Kenya. Mazao hadi gunia kumi yanaweza kuvunwa kwa kila eka lakini changamoto zinazozuia ni mvua duni, utunzi mbaya wa mimea, rutuba duni, nzi wa maharagwe wengi na utumiaji wa mbegu isiyofaa. Mbegu za hali ya juu ya ubora zinahitajika ili kupata mazao tele.

Ishara za mbegu nzuri ya maharagwe

- Yanayofanana
- Uwezo wa kumea
- Zisizo na maradhi yaletwayo kupitia mbegu
- Zisizo na vifaa visivyofaa ndani yake
- Zisizokujana zisizo na ulia na zisizopasuka
- Zisizo oza au kupoteza rangi.



Aina za maharagwe yaliyoimarishwa

KARI katumani wametambua aina nne za maharagwe ambazo hustahimili ukame na zenye mazao ya viwango vya juu kama ifuatavyo.

Katumani Bean I (KAT-BI) - Kathika

- Maua ya rangi ya waridi.
- Huoka maua baada ya siku 30 hadi 31
- Hukomaa baada ya siku 60 hadi 65 na tano.
- Mavuno huwa 1.4 hadi tani 1.9 (kilo 1,400 hadi 1,900 kwa hektari) au gunia 7 hadi 9 kwa kila eka.

- Maharagwe yalio matamu na hayachafui tumbo.
- Hustahimili joto na hukua vyema chini ya Kivuli ya ndizi.

Katumani Bean 9 (KAT B9) - Gacuma

- Huwa na rangi ya waridi.
- Huota maua kwa siku 30 hadi 40.
- Huota maua wakati mmoja.
- Hukomaa kwa siku 60 hadi 65.
- Mbegu huwa rangi nyekundu kasha hudhurungi kiasi zikipikwa na mahindi.
- Mazao hua mifuko 7 hadi 9 kwa eka (1,400 – 1,900 kg/ha).
- Hustahimili ukame kuliko KAT BI.

Katumani X-56 (KAT X-56)


- Mimea ina maua ya rangi ya waridi.
- Huota maua kwa siku 30 hadi 35.
- Hukoma kwa siku 60 hadi 65.
- Mbegu huwa nyekundu, ndefu na mviringo mrefu (oblong).
- Mazao huwa gunia 7 hadi 10 kwa eka au kilo 1,400 hadi 2,000 kwa eka.
- Huzaa zaidi ya KAT/B-I na KAT/B-9.
- Maharagwe mbichi yaliyokomaa hayaathiriwi na mvua nyingi.
- Huiva haraka na ni tamu.

Katumani X-69 (KAT X-69)



- Zina maua meupe.
- Huota maua kwa siku 30 hadi 35.
- Mbegu ni ndefu, oblong na rangi ni kama ya rosecoco lakini zenye wekundu tititi.
- Huinama kwa ajili ya uzito wa mazao yake na urefu wa mmea wenyewe.

- Hustahimili kutu (*Uromyces sp.*), virusi vya kawaida vya maharagwe *mosaic (CBMV)* na huvumilia maradhi ya *angular leaf spot* na *charcoal rot*.

KAT BI (Kathika)



KAT B9



KAT X56



KAT X69

Mbinu mwafaka za ukuzaji

- Tayarisha ardhi kwa kuchimbua udongo hadi uachiliane wiki 2 hadi 4 kabla ya mvua kunyesha ili vipande vya mimea kwa mchanga vioze.

Unaweza kutumia jembe, plau na tingatinga kwa kuchimbua.

Wakati wa kupanda

Ni muhimu kupanda mara tu mvua inyeshapo au milimita 30 za mvua kupatikana.

Kiasi cha mbegu

Panda kilo 16 hadi 20 kwa eka (40 -50 kwa hektari (mbegu mbili kwa shina).